**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

**CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI**

**Ndugu**..............................................

**Anuani**..:..........................................

**YAH: UDAHILI WA KOZI ZA ASTASHAHADA YA MSINGI (BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE) KWA MKUPUO WA SEPTEMBA KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026.**

Mkuu wa Chuo Cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (Institute of Rural Development Planning) anakupongeza kwa kuchanguliwa kujiunga na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kwa mwaka wa masomo 2025/2026.

**Kozi zitolewazo zinapatikana kwa ngazi ya Astashahada ya Msingi (Basic Technician Certificate) ni:**

i. Astashahada ya Mipango ya Maendeleo Vijijini (Basic Technician Certificate in Rural Development Planning).
ii. Astashahada ya Maendeleo ya Jamii (Basic Technician Certificate in Community Development)

**Sifa za Mwombaji:**

Mwombaji awe amehitimu **KIDATO CHA NNE** na kufaulu walau kwa kiwango cha alama "D" nne katika masomo **yoyote isipokuwa somo la dini**.

**Muda wa Masomo:**

Masomo ya Astashahada hutolewa kwa muda wa mwaka mmoja kwa mjumuisho wa mafunzo ya nadharia na vitendo (field practical training).

**Kuripoti Chuoni**

Mwanafunzi anapaswa kuripoti Chuoni mwishoni mwa wiki ya Mwezi **Oktoba,** 2025 hadi mwanzoni mwa wiki ya mwezi **Novemba,**2025 pindi watakapopata barua rasmi ya kuchaguliwa na kuwasili na vitu vifuatavyo: -

1. **Vyeti vya masomo**

Mwanafunzi wanapaswa kuwasili na vyeti halisi (original certificates) vya Taaluma na cha kuzaliwa (Zingatia: Chuo kitapokea nakala halisi ya matokeo "valid results slip" kwa waliomaliza 2024 tu)

2. **Ada**

Kwa wanafunzi wa kozi za Astashahada (Basic Technician Certificate, NTA Level 4) wakiwemo wale waliochaguliwa na serikali ada yao ni Sh. 940,000/= katika kozi zote mbili zitolewazo na kituo cha mafunzo (Mwanza).

**Jedwali Na. 1:** Mchanganuo wa ada kwa kozi za Astashahada ya Msingi (Basic Technician Certificate)

| | Siku ya Kuripoti | Baada ya Miezi Miwili | Jumla |
|---|---|---|---|
| Muhula wa Kwanza | Sh. 340,000 | Sh. 200,000 | Sh. 540,000 |
| Muhula wa Pili | Sh. 200,000 | Sh. 200,000 | Sh. 400,000 |
| Jumla Kuu | | | Sh. 940,000 |

3. **Mahitaji mengine**
   i. Bima ya afya Sh. 50,400/= au Kadi ya bima ya afya ya NHIF inayofanya kazi
   ii. Gharama ya maombi ya kujiunga Sh. 10,000/=
   iii. Gharama ya vipimo vya afya Sh. 5000/= (Vipimo vinafanyika kwenye Zahanati ya Chuo)
   iv. Gharama ya hosteli Sh. 350,000/= kwa Mwaka. Gharama ya hosteli italipwa kwa awamu mbili Sh. 175,000/= Muhula wa Kwanza na Sh. 175,000/= Muhula wa Pili.
4. Malipo yote yatafanyika kwa **CONTROL NUMBER** zitakazotolewa kwenye mfumo wakati wa usajili
5. Wanafunzi watajigharamia gharama za chakula, shajala (stationary) na mafunzo ya vitendo
6. Chuoni hakuna sare, ila wanafunzi wanapaswa kuvaa mavazi yanayokubalika kwa mujibu wa miongozo na taratibu za serikali.

**Kwa msaada na maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi:**

Kampasi Mwanza: **0742 001113, 0742 001114, 0748 002460, 0748 002461, 0748 002462, AU 0748000649**

HEAD OF ACADEMICS
INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING
LAKE ZONE CENTRE MWANZA
DATE........
SIGNATURE........

..........................
**Dkt. Fredrick Mfinanga**
**Mkuu wa Taaluma**
**Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini**
**Kituo Cha Mafunzo (Mwanza)**

Igudija Road, 33409 Kitumba, P.O. Box 11957, Mwanza, Telephone: +255 26 2963037, Fax: **+255 282560995**, E-mail: director@irdp.ac.tz, Website: **mwanza@irdp.ac.tz**